# Maswali

1. Ni kwa nini Mungu alibadili jina la Abramu?
2. Kwa sababu gani Mungu alibadili jina la Sarai?
3. Ni watu wangapi walimtembelea Ibrahimu?
4. Walifanana na wanadamu lakini walionekanaje hasa?
5. Je! malaika waliweza kula chakula?
6. Walimwahidi nini Ibrahimu na Sara?
7. Jina la mwana wao alikuwa nani?
8. Ni kwa sababu gani Isaka alikuwa ni mtoto wa muujiza?
9. Isaka alipokuwa na umri wa miaka 18, Mungu alimtaka Ibrahimu amfanye nini Isaka?
10. Ibrahimu aliposema "Mungu atajipatia mwana kondoo", ni nani hasa alikuwa akimtaja?
11. Akiwa tayari kumtoa Isaka, Ibrahimu alionyesha nini kwa Mungu?
12. Tunawezaje kuuonyesha upendo kwa Mungu?


# Majibu

1. Mungu alibadilisha jina la Abramu kama ishara ya kutimiza ahadi zake zote.
2. Mungu alibadilisha jina la Sarai kama ishara ya kutimiza ahadi zake zote.
3. Watu watatu walimtembelea Ibrahimu.
4. Walionekana kama malaika.
5. Ndio, hao malaika walikula.
6. Waliahidi Ibrahimu na Sara mwana (mtoto).
7. Jina la mtoto wao liliitwa Isaka.
8. Isaka alikuwa mtoto wa muujiza kwa sababu alizaliwa baada ya muda mrefu na kwa wazazi wazee.
9. Isaka alipokuwa na umri wa miaka 18, Mungu alitaka Ibrahimu amtolee sadaka kwa kumchinja.
10. Alikuwa akimtaja kondoo wa sadaka.
11. Ibrahimu alionyesha utiifu na upendo kwa Mungu.
12. Tunaweza kuonyesha Mungu Upendo kwa kutii amri zake.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1 Mwaka wa 1**

# 7 Dhabihu ya Isaka



## Marejeo

Mwanzo 22

## Kiini cha somo

Kuonyesha utiifu wa Ibrahimu kwa Mungu na alivyo mpendeza.

## Maneno maalum

1. Majina ilipadilishwa + watu 3 + Sara + mwana (mtoto).
2. Mwana + Isaka + furuha.
3. Mungu alimjaribu Ibrahimu + Isaka + Safari ya siku 3 + kuni, moto na kisu + wapi mwana kondoo + Mungu atapeana.
4. Jenga madhabahu + inua kisu + Mungu anaita + kondoo mume amenaswa kichakani + Isaka akaachiliwa.
5. Ahadi ya Mungu.

**7.1** Mungu alifanya ahadi mahususi kwake. Moja ya ahadi ilikuwa kwamba Abramu na Sarai watakuwa na mtoto. Abramu na Sarai walisubiri kwa miaka mingi. Walizeeka. Lakini hawakupata mwana. Siku moja Mungu alisema na Abramu tena. Mungu alirudia ahadi zake zote kwake. Mungu alibadili jina lake kuwa Ibrahimu. Alibadili jina la Sarai kuwa Sara.

Mapema baada ya hii, Ibrahimu alikuwa ameketi kwenye mlango wa hema lake, akijikinga jua. Aliona watu watatu wakimjia. Akaenda kuwalaki. Ibrahimu akawakaribisha hao watu watatu nyumbani kwake. Akawapeleka kupumzika kivulini mwa mti mkubwa. Akawatawadha miguu yao kwa maji. Kwa haraka Sara akaandaa mlo wa watu watatu. Ibrahimu na hao watu wakaketi chini ya mti kufurahia huo mlo.

"Sara, mkeo yu wapi?" aliuliza mmoja wa hao watu.
"Yumo hemani," Ibrahimu alijibu
"Mwaka ujao Sara atanyonyesha mwana," alisema huyo mtu.

Ndipo Ibrahimu alitambua kwamba hawa watu kweli walikuwa malaika. Walileta ujumbe huu toka kwa Mungu.

**7.2** Ibrahimu na Sara walifurahi sana kujua kwamba watapata mtoto. Hatimaye Sara aliweza kupata mtoto. Wakamwita jina lake ISAKA. Ni kiasi gani walifurahi. Isaka akakua na kuwa mwenye nguvu naye akawa furaha kwao.

**7.3** Mungu aliujaribu upendo na utii wa Ibrahimu tena. Siku moja labda Isaka alipokuwa mwenye umri wa miaka 18, Mungu alimwambia Ibrahimu "Mchukue mwanao wa pekee Isaka, umpendaye. Uende katika nchi ya Moria kwenye mlima mmojawapo nitakaokuonyesha. Huko umchinje Isaka na kunitolea mimi awe sadaka." Ibrahimu alishangazwa. Ni jinsi gani amchinje mwanawe wa pekee? Isaka aliwaletea furaha wote wawili. Alisubiri muda mrefu kuzaliwa Isaka. Jinsi gani Mungu atatunza ahadi zake kama Isaka akifa?

Lakini Ibrahimu alimpenda Mungu sana. Ibrahimu aliamini ya kwamba, mjua yote ni Mungu. Akamtii Mungu. Alirauka mapema asubuhi na kutandika punda wake. Akawachukua watumishi wake wawili, kuni, moto na kisu. Akaanza safari, akiwa na Isaka. Ibrahimu alisafiri siku tatu. Ndipo akafika kwenye mlima Moria. Ibrahimu aliwaambia watumishi wake wasubiri njiani wakati yeye na kijana wakikwea kwenye mlima kuabudu na kuwarudia. Ibrahimu aliamini kwamba Mungu alikuwa na uwezo wa kumfufua Isaka hata katika wafu.

Ibrahimu akamtwisha kuni Isaka. Walipokuwa wakipanda mlimani, Isaka aliuliza, "Baba yangu, kuni tunazo na moto, lakini yu wapi mwana kondoo kwa sadaka?" Kwa imani Ibrahimu alijibu, "Mwanangu, Mungu atatupatia mwana kondoo wa sadaka."

**7.4** Walipofika sehemu iliyochaguliwa, Ibrahimu akajenga madhabahu. Akapanga kuni juu ya madhabahu. Ndipo Ibrahimu alimfunga Isaka. Isaka alikuwa kijana mwenye nguvu na hivyo angeponyoka. Lakini alimtii baba yake. Ibrahimu akamweka juu ya madhabahu. Akainua kisu chake kumchinja Isaka. Ndipo Ibrahimu akamsikia mtu akimwita, "Ibrahimu! Ibrahimu!” Malaika akamwambia Ibrahimu, "Usimuuwe Isaka. Sasa ninajua unamcha Mungu, kwa kuwa hukuzuilia mwanao, mwanao wa pekee."

Ibrahimu alijaa furaha. Mungu alimwachilia Isaka! Ibrahimu akageuka nyuma na kumwona kondoo amenaswa katika kichaka. Akamfungua Isaka. Halafu akamchukua kondoo na kumtolea Mungu, badala ya Isaka.

**7.5** Mungu alipendezwa sana na Ibrahimu. Mungu aliahidi kumbarikia Ibrahimu na kumpa watoto wengi. Watakuwa wengi kuweza kuwahesabu - kama nyota za mbinguni na kama mchanga ulioko pwani. Uzao wake mmoja mahususi atabariki mataifa yote ya duniani. Ibrahimu alifurahi sana. Mwanawe Isaka bado alikuwa hai. Mungu alimpa ahadi kubwa za thamani.